

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Chini ya Pazia la Ugaidi Polisi Watekeleza Mauaji ya Kinyama

Polisi wamewaua kwa kuwapiga risasi mtu mmoja na watoto wake wawili kwenye uvamizi wa usiku katika kaunti ya Kwale Kusini mwa Pwani ya Kenya. Polisi wanadai kwamba Mohamed Rahma Mapenzi mwenye umri wa 41 anayejulikana pia kwa lakabu ya Spanyol, alikuwa gaidi anaye windwa na kwamba ati kwenye uvamizi huo aliwatumia watoto wake kama ngao-binadamu baada ya kuwarushia guruneti maafisa hao! Mke wa Marehemu, bi Mwanahalima Mwachili aliyekuwa na uja uzito wa miezi minane, alipigwa risasi tumboni na mguuni na sasa amelazwa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Msambweni akiwa katika hali mahututi. **Hizb ut-Tahrir / Kenya**, inatuma rambirambi zake za dhati kwa familia na marafiki wa marehemu na kumuomba majeruhi afueni ya haraka.

Kufuatia kitendo hiki cha kikatili, tunapenda kueleza yafuatayo:

Tangu kupitishwa kwa Mswada wa Kupambana na Ugaidi, ni bayana kuwa polisi mara kwa mara wamekuwa wakiteleza mauaji ya watu nje ya sheria, pasi na uchunguzi wa kina wa mambo, wala amri ya mahakama. Polisi wamekuwa wakituhumiwa kuvamia majumba ya washukiwa, wakiwapandikizia silaha na kuwapiga risasi washukiwa. Vipi polisi waliopokea mafunzo wadai kwamba baba mzazi alitumia watoto wake mwenyewe kama kinga kwake dhidi ya risasi?

Ni wakati sasa kwa raia na hasa jamii ya Kiislamu nchini kuitilia shaka hulka hii ya polisi kwani nchi hii kattu haiwezi kuyafungia macho mauaji haya ya kinyama kwa jina la kupambana na ugaidi. Ama wanasiasa wanaojitokeza wakidai kushutumu ukatili huu, hili kihakika si lolote isipokuwa hufanya hivyo kama mawakala tu wa kiserikali na wa mahusiano ya umma.

Tunaeleza kinaga naga kwamba udhalilishaji na unyanyasaji huu unaoshuhudiwa leo, ni miongoni tu mwa maonevu mengi yanayofanywa dhidi ya Waislamu kote duniani na, kwa yakini kamwe hayatokoma hadi pale Waislamu waregeshe faradhi kubwa iliyo telekezwa ya kufanya kazi kwa lengo moja pekee la kusimamisha tena **Khilafah- Ar-Raashidah** kwa njia ya Utume katika mojawapo ya nchi nyingi za Waislamu. Utawala huo ndio pekee ulio na uwezo wa kulinda Waislamu na hata wasiokuwa Waislamu dhidi ya unyama wa aina yoyote ile.

Shabani Mwalimu

Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya